

HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM



TAARIFA KWA UMMA

Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam inapenda kuwakumbusha, kuwaelekeza na kuwasisitiza wananchi kwamba Serikali imezuia matumizi ya mifuko ya plastiki kuanzia **tarehe 01 Juni, 2019.**

Hivyo, wananchi wote katika Jiji la Dar es Salaam, wasafiri na wageni wanaoingia Dar es Salaam mnaelekezwa kuacha kuzalisha, kuuza, kusambaza na kutumia mifuko ya plastiki kuanzia tarehe 01 Juni, 2019.

Kwa atakayekiuka katazo hili adhabu ya faini au kifungo gerezani itatolewa kwa mujibu wa **Kanuni za "Marufuku ya Matumizi ya Mifuko ya Plastiki za mwaka 2019" zilizoandaliwa chini ya Sheria za Mazingira ya Mwaka 2004.**

Wananchi katika Jiji la Dar es Salaam mnaelekezwa kutumia mifuko mbadala na kuwajulisha majirani, ndugu na marafiki zenu kuzingatia katazo hili.

Sipora J. Liana
MKURUGENZI WA JIJI
HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM